

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA

SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA**

NAMBA ZA SIMU

SHULE YA SEKONDARI KINAMBEU,

MKUU WA SHULE: 0788252992/0753996422

S. L. P 48,

MAKAMU M/SHULE: 0766646060/0753339181

KIOMBOI-IRAMBA,

MWALIMU MWANDAMIZI TAALUMA: 0769234730

JINA LA MWANAFUNZI: _____, JINSI: ME

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI
KINAMBEU-HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA-MKOA WA SINGIDA
MWAKA.....**

1.0 UTANGULIZI .

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule yetu mchepuo wa_____. Shule ya Sekondari Kinambeu ni shule ya mchanganyiko, ni shule ya kutwa na hostel kwa kidato cha kwanza hadi cha nne na ni shule ya Bweni (wavulana) kwa kidato cha tano na sita.

2.0 KAULI MBIU, DIRA, DHAMIRA NA TUNU ZA SHULE

2.1 K a u l i mbiu ya shule

Elimu kwa maisha bora (Education for better life).

2.2 Dira ya shule

Kuwa miongoni mwa shule bora ndani ya wilaya, mkoa na Taifa kwa ujumla (To be among the best school in district, region and nation at large).

2.3 Dhima ya shule

Kuweka mazingira wezeshi kwa watumishi na wanafunzi yatakayoweza upatikanaji wa elimu bora (provision of conducive environment to both workers and students that will enhance quality education delivery).

2.4 Maadili ya shule

Ili kuandaa raia wema na wenye tabia njema shule ina tunu zifuatazo: - utii, bidii, heshima, uaminifu, ushirikiano, uwajibikaji, uadilifu, uvumilivu na uzalendo. (obedience, diligence, respect, trustworthiness, teamwork, accountability, integrity, perseverance, and patriotism).

3.0 MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo kando ya Barabara ya Misigiri - Kiomboi umbali wa kilomita 7 kutoka mji wa Misigiri kuelekea Kiomboi ambako ndipo yalipo makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Mji wa MISIGIRI upo kando ya Barabara ya Singida - Igunga. Nauli kutoka njia panda ya Misigiri hadi Kinambeu sekondari ni Tshs 1,000 kwa usafiri wa Bajaji, Noah au Hice.

Kwa wanaosafiri kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kigoma, Rukwa, Katavi, Shinyanga, Katavi na Tabora kupitia Igunga kuelekea Singida, washukie mji

wa MISIGIRI na wapande magari yanayoelekea Mji wa Kiomboi washukie kituo cha Shule ya Sekondari KINAMBEU.

Kwa wanaosafiri kutokea mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Manyara na Kilimanjaro yapo magari ya moja kwa moja hadi Kiomboi, utashukia KINAMBEU Sekondari. Unaweza panda gari lolote linalopita Barabara ya Singida - Igunga na kushuka Misigiri kisha kufika Kinambeu Sekondari kama ilivyoelekezwa hapo juu.

Shule itafunguliwa tarehe.....au kama itakavyoelekezwa na serikali kupitia vyombo vya habari, unatakiwa kufika shuleni tarehe hiyo bila kukosa.

4.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

4.1 MASOMO YANAYOFUNDISHWA

Shule ni ya mchepuo wa sayansi na sanaa. Tahasusi zilizopo kwa sasa ni PCM na HKL. Masomo yanayofundishwa ni pamoja na Physics, Chemistry, Advanced Mathematics, History, Kiswahili, English Language na Historia ya Tanzania na Maadili.

4.2 Sare za Shule.

- (a) Suruali mbili za rangi ya darkblue (chini upana inch 15), mashati meupe mawili 1 mikono mirefu na 1 mikono mifupi, sweta la darkblue pea moja, kizibao cha dark blue, viatu vyeusi (vya kufunga kamba) vya ngozi pea mbili na soksi nyeusi pea mbili.
- (b) Kila mwanafunzi awe na **Tai 2 ndefu** rangi ya dark blue sawa na rangi ya suruali/sweta
- (c) T-shirt ya rangi ya kijivu 1 itavaliwa siku ya ijumaa.
- (d) Suruali 2 za kijivu (shamba dress) chini upana inch 15 na T-shirt 2 za dark.

4.2 Sare za Michezo.

Kila mwanafunzi aje na raba pea moja, tracksuit nyeusi, T-shirt ya blue (jezi ya Taifa stars), bukta nyeusi na soksi ndefu nyeusi za michezo.

5.0 MAHITAJI YA SHULE

5.1 MICHANGO MUHIMU YA SHULE

SN	AINA YA MCHANGO	KIASI
1	Mchango wa Uendeshaji wa Shule	65,000/=
2	Tahadhari	5,000/=
3	Nembo	5,000/=
4	Kitambulisho	5,000/=
Jumla		80,000/=

NB:

i. Kila mwanafunzi aje na **BIMA ya Afya**, shule haina gharama za matibabu kwa wanafunzi, hilo ni jukumu la mzazi, na kwa ambao hawana **BIMA aje na Tshs. 50,400/=** kwa ajili ya BIMA.

ii. Fedha ya BIMA na T-Shirts zitalipwa Shuleni wakati wa kuripotini, **HIVYO FEDHA HIZO ZISIWEKWE KWENYE AKAUNT YA SHULE.**

iii. Fedha ya michango (**Jedwali 5.1**) muhimu ya Shule italipwa yote kwenye akaunti ya Shule ya NMB bank kwa kuandika jina la mwanafunzi husika na si vinginevyo.

JINA LA ACCOUNT: KINAMBEU SECONDARY SCHOOL RECURRENT

ACCOUNT NAMBA: 50601100196.

5.2 MAHITAJI YA TAALUMA

- (i) Rimu mbili (2) A4 aina ya **Double A (80gsm)** kwa mwaka
- (ii) Begi la kubebea daftari na vifaa vingine awapo shuleni.
- (iii) Scientific calculator kwa wanafunzi wa PCM – function 991.
- (iv) Madaftari yanayotosheleza matumizi ya mwanafunzi kwa mwaka mzima (Counter book 10 kuanzia Quire 3)
- (v) Stop watch moja kwa wanafunzi wa PCM
- (vi) Unashauriwa kuja na Vitabu kiada/ziada vinavyoendana na tahasusi yako.

Yafuatayo ni mapendekezo ya aina za vitabu vya ziada vinavyotumika kwa kidato cha tano na sita unaweza tafuta baadhi kwa matumizi yako binafsi:

SN	SOMO	JINA LA KITABU/VITABU
1	PHYSICS	-Principles of Physics by Nelkon 5th Ed. -ABC Modern Physics 1,2. -Roger Muncaster. -S. Chand's, (Class XI, "Principles of Physics". -S. Chand's, (Class XII, "Principles of Physics". -Thom Duncan, "A-Level Physics".
2	CHEMISTRY	- CHAND XI and XII. -A-Level Chemistry Ramsden 4 th Ed. -Organic Chemistry Part I & II. -Inorganic Chemistry Part I & II. -Soil Chemistry. -Physical Chemistry for A-Level. -TIE, (2019), "General Chemistry for Advanced Level Secondary Student's Book Form Five and Six".

		<p>-TIE, (2019) “Inorganic Chemistry for Advanced Level Secondary School Student’s Book form Five and Six”.</p> <p>-TIE, (2019) “Physical Chemistry for Advanced level Secondary School Students Book Form Five and Six”.</p> <p>-TIE, (2019), Organic Chemistry for Advanced level Secondary School Students Book Form Five and Six”.</p>
3	ADVANCED MATHEMATICS	<p>-CHAND Class XI & XII</p> <p>-Pure Mathematics I & II by Back House.</p> <p>-TIE, (2019), “Advanced Mathematics for Advanced Level Secondary Student’s Book Form Five”.</p> <p>-TIE, (2019), “Advanced Mathematics for Advanced Level Secondary Student’s Book Form Six”.</p> <p>-Advanced Mathematics by Tranter.</p>
4	HISTORY I	<p>-Salehe Yasin, (2018), “Themes in African History Paper 1”.</p> <p>-Jeannes Bigirwamungu & George Tumaini, (2011), “Understanding African History-History Paper 1</p> <p>-Notes-Advanced Level Secondary School Education Form Five & Six, Afroplus Industries-Dar es Salaam-Tanzania.</p> <p>-Rodney, W. (1976). How Europe Underdeveloped Africa, Publishing House: Dar es salaam, Tanzania.</p> <p>-Comrade Sh i b i t a l i , “ Contemporary H i s t o r i c a l e v e n t s -</p>
5	HISTORY II	<p>-Salehe Yasin, “Essential in Advanced level History Paper 2”.</p> <p>-Kato A, “Mastering in Advanced level History Paper 2”.</p> <p>-Zisti Kamili, “History 2 Alive”.</p> <p>Comrade Shibitali, “Contemporary Historical events- History paper 2”.</p>
6	KISWAHILI 1	<p>-TET, (2019), “Kiswahili Shule za Sekondari-Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita”.</p> <p>-Jubeck A. Masebo & Nyambari M. Nyangwine, (2016), “Nadharia ya Lugha Kiswahili 1-Kidato cha Tano na Sita”.Dar es Salaam-Tanzania.</p>
7	KISWAHILI 2	<p>-Nyambari Nyangwine “Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita”.</p> <p>USHAIRI</p> <p>-Kimbunga - Haji Gora</p> <p>-Mapenzi Bora - Shaban Robert</p> <p>-Chungu Tamu - Theobald A. Mvungi</p> <p>-Fungate ya Uhuru- Mohamed S. Khatibu</p> <p>-Usiku Utakapokwishwa - Mbunda Msokile</p> <p>-Kufikirika - Shaban Robert</p> <p>-Mfadhili - Hussein Tuwa</p> <p>-Vuta N’kuvute - Shafi A. Shafi</p> <p>TAMTHILIYA</p> <p>-Kwenye Ukingo wa Thim - Ebrahim Hussein Morani - Emmanuel Mboga</p> <p>-Kivuli Kinaishi - Said Mohamed Nguzo Mama - Penina Muhando</p>
8	ENGLISH LANGUAGE I	<p>-Advanced level English Language 1 (Reviewed Students Class notes)</p> <p>-Advanced level English Language 01” by Nicholous Asheli.</p> <p>-Advanced level English Language 01”-Oxford Advanced Learner’s Dictionary.</p>
9	ENGLISH LANGUAGE 2	<p>-Ashel N (2010), “Appreciation of Literary work”.</p> <p>“Stylistic and Communication in English”.</p> <p>LIST OF READINGS PLAYS</p> <p>-Betrayal in the city - Francis Imbuga</p> <p>-I will Mary when I want -Ngugi wa Thiong’o and Ngungi wa Mini</p>

		<p>-The bride - Austin Bukonya Lwanda Magere - Okoiti Omtatah -Black Mamba - John Ruganda NOVEL AND SHORT STORIES -Encounters from Africa - Macmillan Education Limited -The Beautiful ones not yet Born - Ayi kwei Armah -Divine providence - Severin N. Ndunguru A man of the people - Chinua Achebe -The rape of the pearl - Magala Nyago -Varnishing shadows - Namige Kayondo -His Excellency the Head of the State - Danny Sajo A - season of waiting - David Omowale POETRY -Selected Poems - Institute of Education The Wonderful surgeon and other Poems - Charles Mloka</p>
10	HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI	

5.3 MAHITAJI YA VIFAA VYA USAFI, MALAZI NA CHAKULA

- (i) Squeezer (1) kwa PCM.
- (ii) Mfagio (1) wa sakafu (soft bloom) kwa HKL
- (iii) Jembe moja (1) lenye mpini kwa HKL
- (iv) Sabuni ya chooni aina ya Aro lita tano (5) kwa michepuo yote.
- (v) Fyekeo (kwanja) lililonolewa (1) kwa PCM.
- (vi) Shoka moja (1) lenye mpini kwa PCM.
- (vii) Hard broom (1) kwa michepuo yote.
- (viii) Panga moja (1) kwa michepuo HKL.
- (ix) Ndoo moja (1) ndogo zenye mifuniko na galoni ya kutunzia maji ya kunywa kwa michepuo yote.
- (x) Godoro moja (1) (ft 2.5x6)
- (xi) Shuka mbili (2) rangi ya blue bahari na foronya rangi ya blue bahari
- (xii) Chandarua kimoja cheupe (1), pembe nne
- (xiii) Blanket moja na pajama la kulalia.
- (xiv) Vyombo vya chakula:- kijiko, kikombe, bakuli na sahani.

Fomu za: (i) historia ya mwanafunzi, (ii) sheria, kanuni na taratibu za shule iliyoambatana (iii)kiapo cha utii na (iv) uthibitisho wa afya ya mwanafunzi zimeambatanishwa pia. Fomu hizo zijazwe na kurudishwa shuleni wakati wa kuripoti.

Ni **LAZIMA** kila mwanafunzi kufika shuleni na nakala (photocopy) ya **cheti chake cha kuzaliwa, faili** kwa ajili ya kuweka **kumbukumbu** zake muhimu, **picha nne ndogo za passport** na nakala ya result slip yake.

KARIBU SANA KINAMBEU SEKONDARI



**Godfrey Gabriel Yohana
Mkuu wa Shule**



PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
IRAMBA DISTRICT COUNCIL

KINAMBEU SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 48,
KIOMBOI-IRAMBA,
08/05/2026

To The Medical Officer,

Dear Sir/Madam

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine Mr. _____
as to his/her fitness as a fulltime student of this school. May I kindly
request you to fill in, the particulars given in the form here under.

Yours Sincerely,



Godfrey Gabriel Yohana
The headmaster



TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER

1. Blood count (White blood cells)
2. Stool examination
3. Urine examination.....
4. Gestation (for girl only)
5. Venereal diseases.....
6. T.B test.....
7. E.N.T problems.....
8. Defects of the left and right eye.....
9. Defect of the chest.....
10. Does he/she have any CHRONIC or FAMILY diseases Eg. Epilepsy,
sickle cell etc.

I have examined Mr. _____ and I certify that he/she
is physically **fit/not fit** to pursue student duties as stated above.

.....
Name and Signature

.....
Stamp

.....
Date

**OFISI ZA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA
SHULE YA SEKONDARI KINAMBEU
FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi _____
2. Tarehe ya uzaliwa _____ wilaya _____
3. Mahali alipozaliwa _____
4. Dini (Mkristo/Muislamu) _____
5. Matatizo ya kiafya (kama yapo) _____
6. Jina la baba mzazi _____ Yuko hai/amefariki _____
7. Kama amefariki taja mwaka aliofariki _____
8. Jina la mama mzazi _____ Yuko hai/amefariki _____
9. Kama amefariki taja mwaka aliofariki _____
10. Wewe ni mtoto wa ngapi kuzaliwa kwenye familia yenu _____
11. Jina la mlezi (kama haulelewi na wazazi) _____
12. Anuani ya mzazi/mlezi _____
13. Jina la kijiji utokacho _____ kata _____
14. Kazi afanyayo mzazi/mlezi _____ Namba ya simu _____
15. Sehemu anakofanyia kazi _____
16. Kazi ambayo ungependa kufanya baada ya kumaliza masomo _____
17. Habari zingine za jamaa wa familia _____

SN	JINA	UHUSIANO	KAZI YAKE	SIMU
1				
2				
3				
4				

18. SAINI YA MZAZI/MLEZI _____ TAREHE _____

SAINI YA MWANAFUNZI _____ TAREHE _____



**Godfrey Gabriel Yohana
Mkuu wa Shule**



OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA
SHULE YA SEKONDARI KINAMBEU
SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule ya Sekondari Kinambeu inaendeshwa kwamujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Kijana anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(i) Nidhamu ni jambo la muhimu kwa kila mwanafunzi. Ili kuonesha nidhamu kila mwanafunzi ni lazima afanye yafuatayo:

- ✓ Kuwa na **Heshima** kwa watu wote, wakubwa kwa wadogo
- ✓ Kuwa na **Ushirikiano** na wanafunzi wenzake, walimu, watumishi wasio walimu na jamii kwa ujumla.
- ✓ Kutokufanya **Makosa** ambayo yanaweza kumsimamisha ama kufutwa shule.
- ✓ Kuvaa **Mavazi ya heshima** wakati wote awapo shuleni na nje ya shule.
- ✓ Kuwa na **Utii** (kwa amri halali) kwa viongozi, walimu, watumishi wasio walimu, wazazi na jamii kwa ujumla.
- ✓ Utunzaji wa Mali zake binafsi, na mali za shule
- ✓ Uvumilivu kwa wanafunzi wenzake, walimu na watumishi wasio walimu.
- ✓ Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- ✓ Ni lazima mwanafunzi aheshimu na kukubali tofauti za kidini kiutamaduni na kisiasa zilizomo katika jumuiya yetu

(ii) Mahudhurio ni jambo la muhimu pia kwa kila mwanafunzi. Kila mwanafunzi anapaswa kufanya yafuatayo:

- ✓ Kutokuwa **mtoro** kwa Kuhudhuria shuleni kila siku (siku 194) za masomo.
- ✓ Kutimiza **wajibu** wake kama mwanafunzi awapo shuleni kwa kusoma kwa bidii.
- ✓ Kufuata **Ratiba ya shule** wakati wote bila kuzembea.
- ✓ **Kuwahi** shuleni kila siku za masomo saa 12:30 asubuhi.
- ✓ Kila mwanafunzi anapaswa kutii **Wito wa dharura**, kwa kuhudhuria mahali alipoitwa.

(iii) Sare za Shule ni jambo la muhimu. Kila mwanafunzi ni lazima:

- ✓ Azingatie kuwa na **Aina sahihi za sare za shule** kama alivyoelekezwa katika barua ya kujiunga na shule.
- ✓ Azingatie **Matumizi sahihi ya sare za shule**. Uvaaji wa mlegezo (kata K) hauruhusiwi.
- ✓ Azingatie **aina ya Mshono wa sare** ulioelekezwa. Suruali za kubana (modal) kwa wavulana haziruhusiwi. Ukibainika umevaa suruali ya kubana, itachanwa kwa mkasi ama wembe.

(iv) **Usafi**

- Kila mwanafunzi ni lazima awe **msafi wa Mwili** wakati wote.
- Kila mwanafunzi ni lazima **avae Mavazi safi** wakati wote.
- Kila mwanafunzi ni lazima ahakikishe **Mazingira** (vyumba vya madarasa, vyoo, mabweni, jiko, ofisi za walimu n.k) ya shule ni safi.

Yafuatayo ni Makosa Yanayoweza Kusababisha Mwanafunzi Kufukuzwa Shule.

- (i) Wizi
- (ii) Kumiliki na kutumia simu bila ruhusa awapo shuleni.
- (iii) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
- (ii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama **vile uvutaji bangi, cocane, mirungi, kubeli nk.**
- (iii) Makosa mengine ya Jinai
- (iv) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake/mtumishi, kutukana/kutukanana na mwanafunzi mwenzake/mtumishi
- (v) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
- (vi) Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa
- (vii) Kuoa au kuolewa.
- (viii) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
- (ix) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
- (x) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
- (xi) Kukataa adhabu halali **kwa makusudi.**

KIAPO CHA UTII

Mimi _____ ambaye ni mwanafunzi wa shule ya

sekondari Kinambeu, nimesoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoielezwa hapo juu. Naahidi kwa hiari yangu mwenyewe, nikiwa na akili timamu na bila kushurutishwa na mtu yeyote kuwa **nitatii**. Na endapo nitathibitika kuwa nimekaidi sheria, kanuni na taratibu hizi, uongozi wa shule usisite **kunichukulia hatua stahiki**. Mwenyezi Mungu nisaidie.

Jina la mwanafunzi

Saini ya mwanafunzi

Tarehe

Jina la mzazi/mlezi

Saini ya mzazi/mlezi

Tarehe



Godfrey Gabriel Yohana
Mkuu wa Shule

